# NYOTA YA MASHARIKI

*Bernard Mukasa*




2.Sirudi kwa njia, yake Herode
Anakuvizia, kila upande
Wivu unamjia, kakunja konde
Lakukuzuia, juu usipande
Ni kama Kaini, mwua Abeli
Au Raubeni wa Israeli
Waliotamani, kuzika hali
Ya wadogo duni, kwake Jalali

3.Ninakuombea, usife Moyo
Maana dunia, si rafikiyo
Wewe fuatia, za Kristo nyayo
Aliyekufia, kwa mizigoyo
Wa ulimwenguni, watakufumba
Wazuri machoni, Moyo mwembamba
Hawatatamani, uitwe Mwamba
Ni wivu moyoni, unawasomba



# NYOTA YA MASHARIKI

*Bernard Mukasa*

